American Journal of
**Education and Practice**
(AJEP)



# UCHUNGUZI WA UUNDAJI WA VITAMBULISHO VYA UTAIFA KATIKA TAMTHILIA YA MSTAHIKI MEYA

*Margaret June Achieng` Mung`ala*
*Dkt. George Obara Nyandoro, Uzamifu*
*Dkt.Charles Nyandoro Moochi, Uzamifu*

AJPO

American Journal of Education and Practice
ISSN 2520 - 3991 (online)
Vol.4, Issue 1, p 60 -71, 2020
www.ajpojournals.org

# UCHUNGUZI WA UUNDAJI WA VITAMBULISHO VYA UTAIFA KATIKA TAMTHILIA YA *MSTAHIKI MEYA*

**Margaret June Achieng` Mung`ala**
Idara ya Lugha, Isimu Na Fasihi
Chuo Kikuu Cha Kisii, Kenya
magjunny@gmail.com

**Dkt. George Obara Nyandoro, Uzamifu**
Idara ya Lugha, Isimu Na Fasihi
Chuo Kikuu Cha Kisii, Kenya

**Dkt.Charles Nyandoro Moochi, Uzamifu**
Idara ya Mtaala, Ufundishaji Na Nyenzo za Kufundishia
Chuo Kikuu Cha Kisii, Kenya

**IKISIRI**

Utafiti huu ulichunguza uundaji wa vitambulisho vya utaifa katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, Arege (2009).Tamthilia ni kazi ya kidrama na ya kimaongezi ambayo huigizwa mbele ya hadhira au ni kazi iliyoandikwa ili kusomwa na hadhira. Isitoshe maagizo haya huakisi hali halisi katika jamii. Lengo kuu la kutunga tamthilia ni kuadilisha na kuwawezesha wananchi kutambua baadhi ya mambo yanayotendeka katika jamii halisi kwa kuwa, fasihi ni ukweli wa maisha. Vitambulisho ni sifa, hisia ama imani ambazo humtofautisha mtu au kabila au raia wa nchi fulani na nyingine. Huku utaifa ni hali ambapo wananchi wote hujitambua kuwa sawa katika taifa fulani na hushiriki kwa pamoja katika kuleta amani na maendeleo taifani mwao.Utafiti huu ulinuia kujibu swali lifuatalo, Kwanza, dhana ya vitambulisho vya utaifa vimejitokezaje kwa mujibu wa tamthilia ya *Mstahiki Meya?* Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhistoria mpya ikishirikiana na nadharia ya utaifa. Umuhimu wa utafiti huu ni kwamba, utaongeza maarifa katika nadharia na mbinu za uhakiki wa tamthilia za Kiswahili nchini Kenya, kwa kurejelea na kuweka wazi vitambulisho vya utaifa, pia utaweza kutumika katika taaluma ya fasihi hususan tamthilia, kama marejeleo na itawasaidia wanafunzi na watafiti watakaotaka marejeo ya tamthilia ya Kiswahili nchini Kenya ili kuweka wazi vitambulisho vya utaifa na jinsi vinavyojitokeza katika tamthilia, vilevile ni malighafi kwani utatoa mchango mkubwa katika historia ya tamthilia nchini Kenya na kutajirisha maktaba ya chuo kikuu cha Kisii. Aidha, tume ya utangamano wa taifa nchini Kenya (NCIC), itagundua umuhimu wa fasihi kupitia tamthilia, katika uundaji wa vitambulisho vya utaifa inayoendeleza utangamano nchini hivyo basi itawawezesha kufadhili tafiti zitakazonuia kushughulikia suala hili. Uchunguzi huu ulifanywa maktabani. Muundo wa utafiti uliotumiwa ni utafiti elezi. Kwa hivyo matokeo yaliwasilishwa kupitia maelezo.

**Usuli wa utafiti**

Hii ni tasnifu ya utafiti ambayo ilinuia kuchunguza uundaji wa vitambulisho vya utaifa jinsi katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, iliyoandikwa na Timothy Arege (2009). Tamthilia ni mojawapo ya tanzu kuu katika fasihi andishi ambao hutegemea mazungumzo na uigizaji ili kuwasilisha ujumbe wake (Wamitila, 2008)). Huu ni utanzu ambao huandikwa kwa mtindo wa mazungumzo ya wahusika ambao hukuza tendo kuu la kidrama. Ni chombo cha mawasiliano na pia cha kuwazindua watu juu ya mwelekeo wa mambo tofauti yanayotokea katika jamii (Wafula, 1999). Hii ni kusema kuwa kupitia kwa tamthilia ujumbe fulani unaweza kuwasilishwa kwa hadhira.

Madhumuni ya kutunga tamthilia ni kwa ajili ya kutendwa na kuonyeshwa (Wamitila,2008). Kwa hivyo sifa ya kwanza ya tamthilia ni kwamba hutawaliwa na uwasilishaji kupitia matendo na usimulizi. Usimulizi ambao ni wa aina tatu. Kwanza kuna usimulizi unaopatikana kupitia maelekezo ya jukwaani ambayo huandikwa katika mabano, vilevile kuna matumizi ya msimulizi (mbinu ya kiutendi au kiepiki upatikanao katika muundo wa drama) ambaye husimulia matukio yanayopatikana katika tamthilia. Isitoshe, mazungumzo ya wahusika yanaweza kutekeleza dhima ya kusimulia kisa kikuu katika kazi inayohusika. Sifa ya pili ya tamthilia ni kwamba ina maelezo ya jukwaa itakavyoonekana kuhusu mambo ya samani, mapambo, taa – yaani uwashaji na uzimaji wake, vielelezo na visaidizi. Tatu, kuna maelezo ya muziki au ngoma au sauti au nyimbo ikiwa itahitajika. Nne kuna maelezo ya wahusika kuhusu mavazi, uzungumzi nafsi kwao, hisia na matendo yao. Hatimaye kuna mgawiko wazi wa matendo na matukio kwa mujibu wa sehemu na sura mbalimbali. Kigezo kikuu cha tamthilia ni uwezo wake wa kuwasilishwa jukwaani. Kama sanaa ya lugha, suala la uigizaji na utendaji kwenye jukwaa ni muhimu sana na ni lazima lichunguzwe katika uchambuzi wowote, hii ni kwa sababu hadhira hushuhudia na kuona tukio likiendelea kuliko kusoma au kusikiliza tu kama ilivyo katika sanaa zingine, (Wamitila, 2008).

Hivyo basi lengo kuu la kutunga tamthilia ni kuwawezesha wananchi kutambua baadhi ya mambo mazuri na mabaya yanayotendeka katika jamii ili kuadilisha, kufunza, kutumbuiza, kuhamasisha, kuonya pamoja na kuelekeza. Katika uhakiki wa kazi za fasihi hususan tamthilia kipengele cha maudhui hushughulikiwa. Maudhui ni jumla ya mawazo yote yanayozungumziwa pamoja na falsafa ya mwandishi juu ya mawazo hayo. Hujumuisha mawazo vilevile mafunzo mbalimbali yaliyomsukuma msanii hadi akatunga na kusanii kazi fulani ya kifasihi.Vipengele vya maudhui ni pamoja na dhamira, migogoro, falsafa, ujumbe na msimamo wa mwandishi (Arege, 2007).

Kipengele cha lugha ni muhimu sana katika kazi yoyote ile ya sanaa ya fasihi. Matumizi ya lugha hufanya kazi fulani ionekane tofauti na nyingine au hutofautisha kazi ya sanaa ya Kiswahili na ile isiyo ya fasihi. Lugha ndio malighafi ya kubuni kazi ya fasihi, kwani fasihi ni kazi ya sanaa inayotoa maudhui yake kwa kutumia lugha ya maneno (Msokile,1993). Kipengele hiki cha lugha kimegawika katika sehemu mbili kuu. Kwanza ni mbinu za lugha au tamathali za usemi ambazo hutumiwa na waandishi wa fasihi kutilia nguvu na msisitizo katika sauti na maana, aidha hutumiwa ili kuipamba kazi ya sanaa ya fasihi kwa kuongeza utamu wa lugha. Pili ni mbinu za kisanaa au mitindo ya uandishi ambayo hufanya kazi ya fasihi kuwa tofauti kwani kila mwandishi ana njia yake maalumu ya kuwasilisha ujumbe wake.Yaani, kila msanii ana mitindo yake ambayo ni tofauti na ya wengine, (Juma, 2001)

Hariyanna (1995) anadai kuwa utaifa ni hali ya kuwa na ufahamu juu ya kitambulisho kimoja baina ya wananchi. Hii inachukuliwa kuwa hata watu wawe na makabila, dini, maeneo au ndimi tofauti tofauti wote ni kitu kimoja. Anaendelea kusema kwamba jamii ambayo imeshirikiana pamoja kwa umoja aghalabu hufurahia kuishi kwa amani, uthabiti, maendeleo na hujihusisha katika utendajikazi. Joseph (1999) akimnukuu Smith (1993), anasema kwamba utaifa ni itikadi ya mtu kupenda taifa lake kupita kiasi pamoja na watu wake na msingi wake ni uhusiano wa kijamii, kidini na imani wala sio kuwageuza watu wawe na mienendo sawa ya maisha

Lengo hili la kustawisha utaifa, uzalendo na utangamano ni miongoni mwa madhumuni yanayopatikana katika ripoti ya sheria ya Kenya kupitia kifungu nambari 12 ya mwaka wa 2008, sehemu ya pili na ya tatu. Hivyo basi, utaifa ni ajenda muhimu katika kamati ya kudumu ya (NCIC) iliyoundwa Feburuari, 2008 na tume ya kitaifa na uwiano chini ya uwenyekiti wa Mheshimiwa Kofi Annan, na kutiwa sahihi tarehe Februari 28, 2008. Mkataba huu uliwahusisha Mheshimiwa Rais Mwai Kibaki wa chama cha PNU pamoja na Mheshimiwa Raila Odinga, kinara wa ODM. Kamati hii iliundwa baada ya ghasia za uchaguzi zilizoshuhudiwa nchini Kenya mwaka wa 2007-2008. Zahama hizi zilisababisha vifo zaidi ya watu 1500, uharibifu wa mali usiokadirika na wakenya takribani 400,000 kuachwa bila makao, (Mwangi, 2012). Hili ni dhihirisho kamili kwamba nchi ya Kenya wakati huu bado haikuwa imepata sifa za kuweza kuitwa taifa kwani hali hii ilihatarisha na kuvuruga utaifa.

Lengo kuu la (NCIC) ni kuleta maridhiano nchini, ili raia wote wawe na utangamano wa kudumu taifani mwao.Tume hii ilipiga marufuku kulinganishwa kwa makundi ya kikabila ama kumbughudhi mtu kwa msingi ya kikabila. Kwa kufanya hivyo taifa lilitambua kwamba bila ya kuwepo kwa vitambulisho vya utaifa maendeleo hayapatikani.

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uhistoria Mpya ambayo iliasisiwa na Stephen Greenblatt (1980) na kuimarishwa zaidi miaka ya tisini na.Wanahistoria Mpya wanatambua nafasi kubwa na muhimu inayochukuliwa na muktadha wa kihistoria katika usomaji au uhakiki wa kazi za fasihi. Isitoshe, Nadharia ya Utaifa ilitumiwa vilevile katika utafiti huu. Mwasisi wa nadharia hii ni Ernest Gellner (1964). Nadharia yake ilijaribu kueleza vigezo vinavyojenga utaifa. Aliungwa mkono na Thomas H.Eriksen mwaka wa (2002) ambaye alijaribu kufupisha hii.

Uteuzi wa mada uliongozwa na sababu kadhaa za kiusomi. Kwanza, suala la vitambulisho vya utaifa katika tanzu wa tamthilia halijashughulikiwa sana na wahakiki wengi. Japo wengi wamehakiki maudhui au fani tu bila la kuzihusisha na uundaji wa vitambulisho vya utaifa katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, kama vile Were (2012), Ndege (2013), Okwena (2013). Kutokana na tafiti hizi iligundulika kwamba mada hii haijashughulikiwa moja kwa moja , hivyo basi kuacha mwanya wa utafiti ulionipa ari ya kutaka kuuziba kwa kueanya utadfiti huu.

**Suala la utafiti**

Utafiti huu ulichunguza uundaji wa vitambulisho vya utaifa jinsi katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* (2009). Japo kuna tafiti nyingi ambazo zilishughulikia tamthilia kama vile, Khamis (2015) alihakiki kuhusu Usimulizi katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo na Mstahiki Meya*, Were (2012) na Ndege, (2013) wameshughulikia maudhui na fani katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, Kohl (2010) alitafiti kuhusu Utaifa Guinea Bissau baada ya uhuru. Naye Namasaka (2009) alitafiti

kuhusu Matumizi ya lugha ya kienyeji redioni na utangamano wa taifa, huku Wanyonyi (2016) akihakiki kuhusu uasi wazi wa maudhui katika tamthilia teule Kenya.Tafiti hizi hazijashughulikia moja kwa moja kipengee cha vitambulisho vya utaifa katika tamthilia. Kwani zilijikita tu katika uhakiki wa lugha, maudhui na wahusika kwa upekee bila ya kuzihusisha na uundaji wa vitambulisho vya utaifa. Hivyo basi utafiti huu ulichochewa na hamu ya kutaka kuuziba mwanya huu kwa kuchunguza uundaji wa vitambulisho vya utaifa katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*.

## MAPITIO YA MAANDISHI

### Dhana ya Kitambulisho cha Utaifa

#### Kitambulisho

Longhorn (2011) inaeleza kwamba kitambulisho ni sifa, hisia, ama imani ambazo humtofautisha mtu fulani na mwenzake. Eralp (1997) anasema kwamba kitambulisho kina maana ya uwepo na kukubaliwa kwa mtu. Anaendelea kusema kwamba dhana ya kitambulisho kwa kawaida huwa na elementi mbili:

- Kitambuliwa
- Kitambua

Kitambuliwa humwakilisha mtu binafsi na huwakilishwa na nafsi ya kwanza katika umoja kama ‘mimi’ au ‘sisi’ katika wingi. Aidha kitambua, husimamia jamii nzima na huwakilishwa na nafsi ya tatu katika umoja kama ‘nyinyi’ au ‘wao’ katika wingi. Kwa hivyo, mwanazuoni huyu anasema kwamba kitambuliwa ni finomena ya kisosolojia ambayo huibuka kupitia kwa michakato ya utangamano na ‘wao’ au utengano na ‘wao’. Mtu binafsi hujiamulia mwenyewe kuendeleza tabia, amali na mienendo ya jamii ambamo anaishi ili kujipa utulivu mwafaka wa kisaikolojia na wa kimazingira. Ili kupata kitambulisho, mtu ni sharti ajitambulishe na mtu mwingine ili aonekane kuwa amefanana na mtu huyo wa pili.

#### Kitambulisho cha Ukabila

Tuki (2014), inaeleza kabila kuwa ni kikundi cha watu wanaohusiana kupitia lugha, mila, desturi, na utamaduni uliosawa. Maelezo haya yangejumuisha mpaka wa ardhi, uhusiano wa kiukoo ndiposa maana iwe kamilifu. Isitoshe, ukabila unaelezwa kuwa matendo au fikra za mtu za kuthamini kabila lake tu na kuwabagua watu wa makabila mengine (Eriksen , 2002). Anaendelea kusema kwamba ukabila ni uhusiano baina ya makundi tofauti ambayo yanaonekana au kutambuliwa kuwa na tofauti za kiutamaduni. Katika msingi wa kisosholojia makundi haya yana mipaka ya ardhi, lugha, siasa na utamaduni ulio tofauti. Hivyo basi mwanadamu hujitambua kuwa mmoja wa makundi haya kupitia maamuzi yake binafsi, huku tabia zake ni sharti zilingane na za kabila fulani ili akubalike. Eriksen akimnukuu Worsley (1984) anasema kwamba vitambulisho vya ukabila vinaweza kukuzwa au kubadilishwa huku vipya vikichipuka na kukubaliwa iwapo vina umuhimu katika kabila fulani. Kulingana naye utamaduni sawa si msingi wa kitambulisho cha ukabila bali kuna siasa, matukio ya kihistoria pamoja na utamaduni pendwa vinavyodhihirisha utambulisho wa ukabila. Hii ina maanisha kuwa si lazima mtu azaliwe katika kabila mahususi ili atambuliwe bali anaweza kujitambulisha na kabila fulani kupitia mambo kama vile biashara, ndoa, siasa na kadhalika. Eriksen (2002) anasema kwamba

utaifa huweza kutokana na jamii yenye makabila mengi kwa sababu vitambulisho vya utaifa huweza kuundwa pasipo kuegemezwa kwa kabila fulani mahususi au mipaka iliyo bainifu. Haya huwezekana iwapo viongozi na wasomi katika jamii wataipigia debe finomena hii ya uundaji wa vitambulisho vya utaifa (Gellner, 1964).

**Taifa**

Kamusi ya Tuki (2014) inaeleza taifa kuwa ni jamii ya watu wanaoishi katika nchi moja na wanaoungana kupitia matukio ya kihistoria, mfumo wa uchumi na utamaduni chini ya uongozi wa serikali moja. Maelezo haya yana upungufu kwani si lazima watu waishi katika nchi moja ili kupata hadhi ya kuwa taifa bali ile hisi ya utangamano na usawa inafaa iongezwe katika kuelezea maana ya taifa.

Breuilly (1993) anaeleza maana ya taifa kupitia mtazamo wa kimawasiliano kwamba taifa ni mfumo wa ndani ulioendelea wa mawasiliano ambao hujenga hisia ya kitambulisho sawa miongoni mwa watu tofauti. Alter (1994) anasema kwamba taifa huwakilisha eneo ambalo lina uhai, linaloongozwa na hatima ya mwanadamu katika wakati uliopo na wakati ujao. Hivyo basi mtu binafsi au watu watajitambua kwa unyenyekevu kupitia masuala ya kihistoria, kitamaduni na kisiasa. Alter (1994) akimnukuu Deutsh anasema kwamba taifa ni jamii iliyozinduka kisiasa na ambalo linaweza kuwasiliana wenyewe kwa wenyewe iwapo watu wako mbali au karibu kuhusu masuala mbalimbali. Uwezo wa kuwasiliana hufaulu sana iwapo jamii itatumia lugha moja, dini na imani sawa, kumbukumbu ya kihistoria inayolingana pamoja na utamaduni sawa ili kuendeleza maana iliyo na mantiki.Taifa ni jamii iliyokumbwa na mabadiliko ya kihistoria na hatimaye kuwa imara Stalin (1913). Anaeleza kuwa taifa hili huwa ni jamii yenye lugha, jamii yenye mipaka, jamii yenye maisha ya kiuchumi na pia ni jamii yenye muundo wa kisaikolojia inayodhihirika kupitia utamaduni. Vilevile, Alter (1994) akimnukuu Meinecker (1952) anasema kwamba taifa la kisasa limejengwa juu ya msingi wa usawa. Hivyo basi, anatoa aina mbili za taifa.

Kwanza, kuna taifa la kisiasa ambalo linajengwa kupitia kwa nia au maamuzi huru na unyenyekevu wa raia kwa taifa, yaani demokrasia. Mfano; mataifa ya Ufaransa, Uingereza na Marekani.Wananchi wa mataifa haya hujitambulisha kupitia vyama vya kisiasa, kura ya maoni, uchaguzi na kadhalika. Kila mwananchi ana uhuru wa kujichagulia chama mahususi cha kisiasa kwa sababu ya manifesto yake.

Pili, kuna taifa la kitamaduni ambalo huundwa kupitia kwa urathi wa kitamaduni kama vile lugha, makazi, dini, mila na historia sawa. Si lazima pawe na dola au masuala ya kisiasa katika taifa hili, bali urazini wa umoja husababisha hisia za utangamano. Hapa raia hana uhuru wa kusema anatoka taifa gani bali utaifa huelezwa kupitia matukio ya kihistoria na mambo ya kihalisia ambayo humzingira mwananchi punde tu anapozaliwa.

Mtazamo mwingine hueleza taifa kuwa ni jamii ya kufikirika kisiasa (Anderson, 2006). Ni ya kufikirika kwani raia wa hata taifa dogo sana hawawezi kujuana wote, kuonana hata kuingiliana mmoja na mwenzake katika masuala mengi japo wao wanashirikiana kimawazo au kifikra. Kwake mtu anaweza kualikwa katika jamii hii ambapo taifa lilichipuka kupitia kwa lugha wala sio kwa kuzaliwa. Pia utamaduni huweza kumbagua mtu katika taifa fulani, lakini kitu ambacho

huleta utangamano thabiti katika jamii hii ni sauti kupitia kwa vigezo kama vile nyimbo, ushairi na wimbo wa taifa. Lugha huwa ni chombo imara cha kitambulisho kwani mtu hukumbana nayo kutoka kuzaliwa kwake hadi anapokufa.

**Dhana ya Utaifa**

Utaifa ni mchakato ambao huleta pamoja watu wa itikadi, tamaduni, imani, kabila na tabaka tofauti tofauti ili kuunda taifa moja, (Muliro, 2012). Ni hali ya kuwa na amani, hali ya kuwa sawa (Longhorn (2011). Naye Ghurye (1968) anasema kuwa utaifa una elementi mbili kuu: ya kisiasa na ya kijamii. Jega (2002) anaongezea mwelekeo wa Ghurye uzani anapoeleza kwamba elementi ya kijamii huwafanya raia wa nchi fulani kujiona kuwa sawa kwa vile wameunganishwa kupitia historia moja, itikadi na maadili sawa, hisia sawa za kiuzalendo na umoja ambayo imepiku tamaduni na matamanio tofauti miongoni mwao. Naye Njengere (2014) anaongeza kwamba raia katika taifa lililo na utangamano hujifunza kuishi pamoja bila kukiuka haki za kibinadamu, huishi kwa amani na furaha kwa kuheshimu tamaduni za kila mtu zilizo tofauti. Maoni haya yamekubaliwa na Brubaker (2004) ambaye anasema kwamba japo makabila huwa tofauti, utaifa huathiriwa na jinsi makabila haya hujiangalia na kujichukua kupitia masuala ya kitamaduni, wanavyong`ang`ania nguvu katika jamii, wanavyotumia mali ya umma, matatizo ya kitabaka na ukosefu wa usawa.

Katika elementi ya pili, Amali (2013) anakubaliana na Jega (2002) kwamba utaifa huendelezwa na viongozi wa kisiasa wanaposhiriki katika masuala ya kuleta usawa wa kiuchumi katika maeneo tofauti wanayowakilisha katika nchi aliyoishughulikia ya Nigeria, bila kupoteza muda mwingi katika mapigano ya midomo.

Pia Hariyanna (1995) anadai kuwa utaifa ni hali ya kuwa na ufahamu juu ya kitambulisho kimoja baina ya wananchi. Hii inachukuliwa kuwa hata watu wawe na makabila, dini, maeneo na ndimi tofauti tofauti wote ni kitu kimoja. Anaendelea kusema kwamba jamii ambayo imetangamana pamoja aghalabu hufurahi kuishi kwa amani, uthabiti, maendeleo na utendaji kazi mwema.

Vilevile, maoni ya Kochhar (1991) Anaeleza kwamba utaifa ni hisi inayowaleta raia wa taifa pamoja. Hii ni hali ya kutambua ukweli kuwa inawezekana pawe na umoja penye tofauti za kiuchumi na kijamii. Kule kuhisi umoja wa kitaifa kwa ujumla kunastawisha utaifa. Anaendelea kusema kwamba utaifa unalenga kuwafanya watu wawe sawa na wala si kuwafanya wafuate mtindo fulani mmoja wa maisha. Anahitimisha kwa kusema kwamba umoja ni suala muhimu katika utaifa.

**NJIA, MBINU NA VIFAA VYA UTAFITI**

Sehemu hii ilishughulikia muundo wa utafiti, eneo la utafiti, njia za utafiti, uteuzi wa sampuli, vifaa vya utafiti, uchanganuzi wa data na hatimaye maadili wakati wa utafiti.

**Muundo wa utafiti**

Muundo wa utafiti ni chombo ambacho huunganisha elementi zote katika utafiti, ni mkondo kwa ujumla wa utafiti (Kombo, 2006). Hali kadhalika kuna maoni kuwa ni ramani ya utafiti ambayo hujumuisha matarajio ya mtafiti kuhusu utafiti, matokeo ya utafiti na matumizi yake, uwezo wa mtafiti kifedha na kiwakati, umbali wa mtafiti na wajibu maswali, tajriba yake kuhusu anaonuia

kutafiti, vikwazo rasmi na zisizo rasmi zinazoweza kumwaathiri (Thomas, 2009). Majibu ya kauli hizi humwelekeza mtafiti katika kuchagua muundo ambao ni mwafaka zaidi. Katika kuchunguza uundaji wa vitambulisho vya utaifa katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* mtafiti alitumia utafiti elezi.

Utafiti elezi hueleza njia inayofaa zaidi na hugusia nadharia tete kwa kujibu maswali yanayohusu utafiti (Mugenda, 2003). Mtafiti alijikita katika kuchunguza vipengele vya uundaji wa vitambulisho vya utaifa katika tamthilia hii na kuongozwa na nadharia ya uhistoria mpya pamoja na ya utaifa. Alishirikisha mitazamo miwili, ya kiuraia na wa uhusiano wa kudumu.

**Eneo la utafiti**

Utafiti ulifanywa kutoka katika tamthilia ya *Mstahiki Meya,* Arege (2009) ili kuchunguza uundaji wa vitambulisho vya utaifa. Pia, mtafiti alisoma vitabu, majarida, tasnifu na nakala za wavuti zilizohusu mada iliyochunguzwa kwa kurejelea dhana ya taifa na utaifa ili kupata maelezo zaidi juu ya vitambulisho vya utaifa.

**Idadiwakazi lengwa**

Ilikuwa katika tawi la fasihi andishi, kipera cha tamthilia, mtafiti alichunguza uundaji wa vitambulisho vya utaifa katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* (2009).

**Uteuzi wa sampuli**

Haiwezekani kusoma na kuchunguza tamthilia zote za Kiswahili ndiposa sampuli hutumiwa. Sampuli ya kimaksudi ilitumiwa na mtafiti, hii ni kwa sababu tamthilia hii imesomwa katika shule zote za upili nchini Kenya na kutahiniwa katika mtihani wa mwisho wa kidato cha nne (KCSE). Hivyo basi, tamthilia hii huenda ikachukuliwa kama mojawapo ya fasihi ya taifa Achebe (1958) kwa sababu ishasomwa na wanafunzi wengi Kenya nzima.Vilevile tamthilia hii ilitungwa mwaka wa 2009, nchi yetu ya Kenya ilipokaribia kupiga kura ya maoni iliyozaa serikali kuu na ya ugatuzi hivyo basi dhana ya vitambulisho vya utaifa haingekosa kushughulikiwa na mwandishi ndiposa mtafiti akateua tamthilia hii.

**Njia za utafiti**

**Utafiti maktabani**

Mtafiti alisoma kwa kina tamthilia ya *Mstahiki Meya,* iliyoandikwa na Arege (2009).

**Mbinu za utafiti**

**Kusoma na kuandika**

Mtafiti alisoma kwa kina ili kuchunguza uundaji wa vitambulisho vya utaifa katika tamthilia ya *Mstahiki Meya.* Vilevile aliweza kusoma vitabu, majarida na hata kudadavua wavuti kwa kusudi la kupata maelezo kuhusu uundaji wa utaifa. Hivyo basi mtafiti alichanganua dhana ya vitambulisho, kueleza namna ambavyo vitambulisho vya utaifa vimeundwa na kuchunguza mbinu za uandishi zinazotumiwa kuunda vitambulisho vya utaifa.

**Vifaa vya utafiti**

Vifaa vya utafiti vilivyotumika katika utafiti huu vilikuwa: tamthilia ya *Mstahiki Meya* Arege (2009), vitabu, majarida na nakala za wanazuoni. Vilevile orodha ya mbinu za lugha na za

uandishi, kalamu, karatasi, tarakilishi pamoja na vikorokoro zake katika kuchunguza uundaji wa vitambulisho vya utaifa katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*.

**Uchanganuzi wa data**

Utafiti elezi ulitumiwa katika kukusanya data hivyo basi matokeo yaliwasilishwa kupitia maelezo na majedwali.

**Matokeo ya utafiti**

**Dhana ya vitambulisho vya utaifa**

**Mtazamo wa uhusiano wa kudumu/kiasili kuhusu vitambulisho vya utaifa**

Wahasisi wa *Primordialism* ama *Perennialism* (uhusiano wa kudumu/asilia) wanasema kwamba taifa ni kitu ambacho ni cha jadi na ina finomena ya asilia. Waasisi wa mtazamo huu ni Edward shills(1981) na Clifford Geentz (1973). Kulingana na Geentz, lugha ilihusishwa na fikra ambayo ilifunzwa kutoka katika jamii, kwa hivyo kila jamii ni lazima iwe na mitazamo tofauti na nyingine inayosababishwa na fikra.

Wataalamu hawa wanaendelea kusema kwamba makundi ya kikabila na ya utaifa huwepo kupitia imani na matendo ya kitamaduni kama vile uhusiano wa kibayolojia na ya kimipaka; ambazo huendeleza uhusiano wa kudumu punde inapoundwa. Ndiposa makundi mawili ya makabila tofauti huweza kupigana na kuuana kwa sababu ya vitambulisho tofauti vya kikabila kwa mfano, Wahutu na Watutsi ni makabila mawili yanayopatikana nchini Rwanda, lakini kwa sababu yaliathirika na mitazamo tofauti ya kiasili kulikuwa na vita vikali vilivyosababisha (mauaji ya Rwanda ya 1994) mauaji ya Warwanda 800,000 ( Jefremovas ,2005)

Wanaounga mtazamo wa kudumu, wanasema kwamba watu wa jamii fulani au taifa hawawezi kuacha kutangamana na wale watu ambao wamefanana nao, watajitambulisha nao hata kama watu hao hawaleti faida yoyote katika maisha yao. Hivyo basi, iwapo kiongozi fulani atatoka katika kabila yao na haleti mabadiliko yoyote katika maisha yao wataendelea kumsifu na kumchagua katika uchaguzi wowote ikiwa upo.

Katika mtazamo huu, wananchi wa taifa fulani hujitambulisha kwa misingi ya pahali pa kuzaliwa, umbo la mtu (rangi ya ngozi, nywele, uso wake) historia ya kundi husika, lugha azungumzayo mtu, utamaduni, ukoo, kabila, familia, rangi, dini, mila na desturi. Haya ni mambo ambayo mtu hawezi akaepuka kukumbana nayo hapa ulimwenguni kwani humuathiri punde tu anapozaliwa na kujikuta katika kabila au jamii fulani.

Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* tunakumbana na wahusika ambao uhusiano wao unaathiri uundaji wa vitambulisho vya utaifa Kupitia kwa uhusiano wa kudumu. Kuna zahanati ambapo kunapatikana wafanyikazi wawili, muuguzi ambaye ni Waridi na daktari ambaye ni Siki.

Siki ambaye ni msomi na anapatikana katika tabaka la kati anawakilisha wananchi wema katika jamii ambao wanatumia uhusiano wa kiasilia kujitambulisha na wananchi wa kawaida, katika tabaka la chini, yaani maskini ili kutetea maslahi yao. Siki anawatetea wagonjwa ili viongozi waweze kuleta dawa za matibabu katika zahanati na kupunguza gharama za malipo ya huduma ya afya wanazopata hospitalini na vilevile haki ya wafanyakazi wa Baraza kuzingatiwa.

Anatumia uhusiano wa kiuzazi, kiukoo, kimpaka, kikabila na kadhalika kuwatetea wananchi wa nchi yake ya Cheneo. Kinyume cha Siki ni kiongozi wa Cheneo ambaye ni Meya anayeitwa Sosi, anawakilisha wananchi waovu ambao hawachangii katika uundaji wa vitambulisho vya utaifa japo ana uhusiano wa kiasilia na wananchi wa Cheneo amekumbwa na ulafi na ubinafsi kwani uongozi wake mbaya unamnufaisha yeye na familia yake na rafikiye Bili, pamoja na viongozi wengine wa Baraza la jiji ambao wanamuunga mkono. Amekuwa kiongozi wa Cheneo baada ya wananchi kumchagua kwa misingi ya ukabila na uhusiano ulio wa karibu kuwaongoza mara tatu, japo uongozi wake unawadhalalisha wananchi wa kawaida anakiri mwenyewe kwamba akisimama mara ya nne kuwania uongozi wa Cheneo bado atachaguliwa. Meya hajawajibika katika uongozi wake kwani fauka ya kuendesha baraza kwa njia isiyofaa, anapotoshwa na washauri wake kuhusiana na maamuzi ya kimsingi katika uendeshaji na mipango ya jiji. Hatima yake ni kudorora kwa miundo msingi na huduma za umma kwa jumla.

**Vitambulisho vya utaifa kupitia mtazamo wa uraia**

Katika taifa la kiraia, utangamano huendelezwa kupitia kwa uraia au "*citizenship*" inayofungamana na uhuru na itikadi ya kisasa. Huendeleza imani ya kisiasa kuhusu uhuru wa kuongea, dini, uanahabari na kadhalika.Waasisi wa mtazamo huu ni Ernest Renan (1882) na Yael Tamir (1993) ambao wanashikilia kwamba mtu yeyote anaweza kuwa raia wa nchi fulani bila kujali dini, kabila, uana, mali yake, rangi yake na kadhalika. Kila mtu ana nafasi sawa kupitia msingi huu wa kujitambulisha na taifa fulani.

Hapa, dhana ya kitambulisho cha utaifa kimerejelewa kupitia mambo kama vile sheria za taifa, katiba, vyama vya wafanyikazi, nembo za kitaifa, mipaka ya kitaifa, kadi za vitambulisho, uanahabari wa kitaifa, afisi za kitaifa, majengo ya kitaifa, bunge la kitaifa, hospitali na shule za kitaifa, uongozi na kadhalika. Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* dhana ya vitambulisho vya utaifa kupitia mkabala wa kiraia imejitokeza kupitia mambo haya.

## HITIMISHO

Matokeo ya utafiti huu uliofanywa yalidhihirisha kwamba vitambulisho vya utaifa vina umuhimu mkubwa sana katika taifa lolote lile. Vitambulisho vya utaifa kama ilivyogunduliwa huchangia pakubwa katika kuendeleza muumano au utangamano wa raia kutoka katika sehemu au makabila tofauti katika taifa fulani, hivyo basi huimarisha uzalendo miongoni mwa raia katika taifa na hii huiwezesha nchi fulani kupiga hatua ya mbele katika maendeleo. Hii ina maana kwamba taifa halitagawanywa kwa misingi ya ukabila, ufisadi, umaskini, migogoro ya mara kwa mara ya wafanyakazi, ghasia za uchaguzi na kadhalika. Isitoshe, taifa litakuwa na nguvu katika kutekeleza maazimio yoyote bila pingamizi.

## MAPENDEKEZO

Utafiti huu umechunguza uundaji wa vitambulisho vya utaifa katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* kwa kutumia nadharia ya utaifa pamoja na ya uhistoria mpya. Mtafiti anapendekeza kuwa tafiti zingine ambazo zitafanywa zinaweza kuangalia kwa kina uundaji wa vitambulisho vya utaifa katika tanzu zingine za fasihi kama vile katika riwaya, hadithi fupi na pia fasihi simulizi nchini Kenya. Mtafiti anapendekeza uhakiki zaidi ufanywe kuhusiana na hali hii kwa kurejelea masuala ya ufisadi, ukabila migomo ya wafanyakazi na mengineyo.

American Journal of Education and Practice
ISSN 2520 - 3991 (online)
Vol.4, Issue 1, p 60 -71, 2020 www.ajpojournals.org

Isitoshe utafiti zaidi kufanywa kuhusiana na tamthilia hii kwa kutumia nadharia nyingine kando na ya utaifa na ya uhistoria mpya. Wizara ya elimu kuidinisha tahakiki ambazo zitashughulikia kwa kina uundaji wa vitambulisho vya utaifa kupitia usomaji na uchambuzi wa kazi yoyote ile ya fasihi katika viwango vyote vya masomo nchini.

**MAREJEO**

Alice, N .Taming the Demon of Kenya's Election Violence:A Strategy for the NCIC Nov 4. 2011

Alter, P. (1994). *Nationalism.* Bristol: J.W Arrow Smith Ltd.

Amali, I. .. (2013). Cultural Pluralism. *Reconstructive education and nation building in Nigeria* .

Anderson, B. (2006). *Imagined Communities Relections on the Origin and spread of Nationalism.* Edinburgh: Quebecor World,Fairfield.

Arege, T. (2007). *Kielezi Cha Tungo.* Nairobi: Focus.

Babbie, R. (2010). *The Practice of Social Research.* Belmont: Wadsworth Centage Learninig.

Bertoncini. (2009). *Outline of Swahili literature.* Leiden: Boston brill.

Breuilly, J. (1993). *Nationalism and the State,2nd Ed.* manchester: Manchester university press.

Chimera, R. (2000). *Kiswahili:Past,Present and future.* Nairobi: NRB.University Press.

D. Njengere. (march 2014). *Role of Curriculum in Fostering national Cohesion and Integration.* Geneva: UNESCO International bureau of education.

Elimu, W. y. (2007). *Secondary school kiswahili syllabus.* Nairobi: k.i.e.

Eriksen, T. (2002). Anthropological Perspective. *Ethnicity and Nationalism* .

Flick, U. (2009). *An Introduction to Qualitative Research 4th. ed.* New Delhi: Sage.

Ghurye, G. (1968). *Social Tension in India.* Bombay: Prakasha.

Hariyanna, M. (1995). *The Essentials of India philosophy.* New Delhi: Motilal.B.

Harrow, K. W. (2001). Research in African Literatures. *Nationalism* , volume 32,number 3.

Jega, A. (2002). Education,Democracy and Nation Building in Nigeria in the 21st century. *African symposium* .

John.N, C. (2009). *Qualitative,Quantitative and Mixed Approaches.* Nebraska: Sage.

Joseph, L. R. (1999). *Recent Theories of Nationalism* .

Joseph, L. R. (1999). *Recent Nationalism theories* .

K.W.Wamitila. (2008). *Kichocheo Cha Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi.* Nairobi: Phoenix.

K.W.Wamitila. (2002). *Uhakiki wa Fasihi:Msingi na Vipengele Vyake.* Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Khahn, J. .. (2004). *Research in Education.* New Delhi: Prentice hall of India.

Kochhar, S. (1991). *The Teacchings of social studies.* New Delhi: Sterling.

Kochhar, S. (1991). *The teachings of social studies.* New Delhi: Sterling Private limited.

Kombo, D. &. (2006). *Proposal and Thesis Writing.2nd ed vol .1.* Nairobi: Paulines P.Africa.

L.T. Muliro, E. ,. (2012). *History and Goverment.* Nairobi: Longman.

Leinwand, G. (1992). *Public Education :American Issues.* UK: Roundhouse.

Longhorn. (2011). *Kamusi ya karne ya 21.* Nairobi: English press ltd.

Manual, T. C. *Guidelines for preparations and Submissions of Thesis and Dissertations.*

Mayring, P. (2004). *Qualitative Content Analysis.* New Delhi: Sage

Milibrand, Ralph (1969), Theory of the State - Instrumentalist and Structuralism

Mohammed, S. A. (1995). *Kunga za Nathari za Kiswahili:Riwaya,Tamthilia na Hadithi fupi.* EAEP.

Mohammed, S. (2000). *Kitumbua kimeingia Mchanga.* Nairobi: Oxford university press.

Moorman, M. (2001). African Literatures. *Of Westerns Women and war:Angolan Ccinema and the Nation* , vol.32,number 3.

Msokile, M. (1993). *Misingi Ya Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: East Africa Education Publishers.

Mugenda, O. M. (2003). *Quantitative and Qualitative Approaches.* Nairobi: Acts Press.

Mwangi, S. (2012). *A History of constitution Making in Kenya.* Nairobi: Media Development Association.

NCIC. (2013). *National Integration and commission.* Nairobi.

Nderitu, A. (2011). Taming the Demon of Kenya`s Election Violence. *A Strategy for the NCIC* .

Njagi, G. (2014). Introduction to the study of literature. *Dept of Kiswahili and African Languages* .

Njogu &Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi,Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nyambu(Ed.), K. (2011). *NCIC Training Manual.* Nairobi: Ministry of justice,National Cohesion and Constitutional Affairs.

Paul.M.Juma. (2001). *Mwongozo wa kiu.* Nairobi: City Book Publishers.

Radhakrishan, S. (2008). *Indian Philosophy.* New Delhi: Oxford unniversity press.

Rossman, C. M. (2006). *Designing qualitative Research 4th ed.* Thousands oaks: Sage.

Scherr, A. (2013). The construction of National Identity. *Migration Background-as a political and scientifically category* .

Semzaba, E. (2003). *Tamthilia ya Kiswahili.* Dar es salaam: chuo kikuu Huria Cha Tanzania.

Smart, F. N. (2001). Research in African Literatures. *Nationalism and the Aporia of National Identity in Fara`s Maps* , vol.32,no.3.

Smith, A. (1993). *National Identity.* london: Penguin books.

SN. (26th July 2015). Nairobi: Nation media.

Stalin, J. (1913). Marxism and the National Question.

Sullivan, J. (2001). African Literatures. *The Question of National Literature for Nigeria* .

Thomas, G. (2009). How to do your Research Project.

Wafula, R. (1999). *Uhakiki wa Tamthilia.* Nairobi: Jomo kenyatta foundation.

Wamitila, K. (2008). *Kanzi ya Fasihi.* Nairobi: Vide Muwa.

Wamitila,K.(2002)Uhakiki wa Fasihi , Misingi na Vipengele vyake.Narobi:Phoenix